

Jina Namba yako

102/1

KISWAHILI

Karatasi 1

(Insha)

Oktoba/Novembe 2015

Muda: Saa $1\frac{3}{4}$

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA KANDARA KIDATO CHA TATU

KISWAHILI

Karatasi 1

Oktoba / Novemba 2015

Muda: Saa $1\frac{3}{4}$

MAAGIZO

1. Andika insha mbili.
2. Insha ya kwanza ni ya lazima.
3. Insha zote zisipungue maneno mia nne. (400)
4. Insha ziandikwe kwa lugha ya kiswahili.

1. LAZIMA

- Umeteuliwa kama katibu wa kamati itakayochunguza kuhusu namna ya kukabiliana na mashambulizi ya kigaidi humu nchini. Andika ripoti kuhusu matokeo ya uchunguzi huo.
2. Mapuuza ndio chanzo cha wingi wa ajali humu nchini. Eleza
 3. Andika kisa kitakachothibitisha methali: Vita vya panzi, furaha ya kunguru.
 4. Maliza kwa maneno “.....maisha haya nisingeyaweza kamwe.”

KANDARA SUB-COUNTY SECONDARY SCHOOLS FORM 3

2015 JOINT EXAMINATION

KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION (K.C.S.E)

Karatasi - 102/1

Octoba/Novemba- 2015

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

Swali la 1

Hii ni ripoti rasmi
Mwanafunzi azingatie yafuatayo

1. Muundo

- a) Aandike kichwa ambacho kitaonyesha ripoti ni ya kina nani/ kamati gani, kuhusu nini, mahali na kipindi cha wakati.
- b) Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari.

2. Utangulizi

- a) Mwanafunzi aeleze kwa kifupi yaliyosababisha haja ya kufanywa utafiti.
- b) Anaweza kitaja wanajopo waliohusika pamoja na muda uliochukuliwa kufanya uchunguzi. Pia, anaweza kutaja atakayewasiliahwa ripiti.
- c) Mwanafunzi ataje mbinu za ukasanyaji data walizozitumia. Mfano, mahojiano, hojaji, upelelezi. kusoma n.k

3. Mwili

Mwanafunzi aweke wazi matokeo ya uchunguzi na yaandikwa kwa mada ndogondogo ambazo zimefafamuliwa vilivyo. Pia, anaweza kuripoti baadhi ya matatizo yaliyowakumba katika uchunguzi wao.

Mwanafunzi anaweza kuzingatia yafuatayo.

- i) Kuelimisha wanafunzi kuhusu madhara ya ugaidi.
- ii) Kukabiliana na ufisadi ili kuzuia magaidi kuiningia nchini na kupata stakabadhi za uraia nchini.
- iii) Kuimarisha usalama katika mahala pa umma. Mfano, vyuoni, vituo vya magari, kanisani, maduka nk
- iv) Kuongeza nafasi za kazi kwa vijana.
- v) Watakaokamatwa wachukuliwe hatua za kisheria.

vi) Kukaguliwa kwa watu kabla ya kujumuika pamoja.

vii) Kuimarisha uzalendo mionganoni mwa wananchi.

viii) Kuwarejesha wakimbizi katika nchi yao.

ix) Kujenga ukuta mpakani kuzuia magaidi kuingia nchini kwa urahisi.

x) Kuwaripoti watu waliotorokea nchi zingine bila fahamu yoyote ya familia yao.

4. Hitimisho

Mwanafunzi arejelee tu matokeo ya uchunguzi.

5. Mapendekezo

- a) Yaorodheshwe kwa nambari.
- b) Yapendekeze suhulisho/hatua za kuchukuliwa.
- c) Jina la mwandishi, sahihi na wadhefa wake uonyeshwe.

6a) Ukiukaji wa sheria za usajiri mfano kubeba abiria zaidi ya idadi inayostahili.

b) Magari kutowekwa vidhibiti mwendo/kuharibiwa.

c) Maofisa wa trafiki hujishughulisha sana na hongo kuliko usalama wa abiria.

d) Magari mengine hayana bima kwa kuwa hayastahili kutumika kubeba abiria.

e) Madereva wengi hawana leseni za kuendesha magari na wengine huzipata kwa njia zisizo halali.

f) Kuendesha gari upande usiofaa

g) Ulevi - Madereva kuwa walevi aidha kutokana na pombe au dawa za kulevya.

h) Wengine hupuuza mawaidha ya daktari wanapoonywa kutoendesha magari aidha baada ya kutumia dawa fulani au kutokana na hali yao ya afya.i)

i) Dereva kuwasiliana kwa simu anapoendesha.

ii) Barabara nyingi huwa mbovu

k) Ishara za usalama wa barabarani kung'olewa na kuuziwa wanaojihusisha na biashara ya

vyuma vikuukuu.

- I) Wanaovuka barabara hufanya hivyo haraka bila kuzingatia sheria au hukataa kutumia vivukio katika barabara kubwa.

Swali la 3

- i) Hii ni methali.
- ii) Mwanafunzi atunge kisa ambacho kitadhihirisha maana ya methali hii.
- iii) Si lazima mwanafunzi aeleze maana ya methali, anaweza kuingilia kisa chake moja kwa moja.
- iv) Kisa cha mwanafunzi kionyeshe madhara ya kutosikizana na namna ambavyo madhara hayo hufaidi wengine.
- v) Mwanafunzi anaweza kuleta dhana ya umuhimu wa umoja na matatizo yanayoambatana na utengano.

Swali la nne

- a) Mwanafunzi atunge kisa ambacho kinaonyesha mateso ya kila aina. Mateso haya yanamfanya kukosa matumaini katika maisha yake.
au
- b) Atunge kisa ambacho kinaonyesha alivyoteseka baada ya kuishi maisha ya heri hapo mwanzoni.
- c) Mwanafunzi atunge kisa ambacho kinaonyesha mabadiliko ya maisha yake na kusababisha kukata tamaa.